

Anza

SHULENI

Umealika marafiki wawili kujiunga na 4-H. Mmoja akasema "Ndiyo". Ongeza nafasi moja.

Una haraka na unamwagilia miche ya nyanya wakati wa chakula cha mchana jua likiwa kali sana. Rudi nyuma nafasi 1.



Nyanya zako zimeshambuliwa na ugonjwa. Tengeneza viuatilifu (dawa ya asili ya kuulia wadudu) kwa kutumia magadi soda na maji na uweke kwenye miche ya nyanya. Nenda mbele nafasi

Umepoteza kitabu cha kumbukumbu za bustani ya darasa lako na haukumbuki jinsi ya kubadilisha mazao kutoka msimu uliopita. Ruka hatua inayofuata.

Klabu yako ya 4-H inaonesha namna ya kutengeneza mbolea ya asili katika mkutano wa mwaka. Nenda mbele nafasi 2.

Umeongoza mchezo wa Kujifunza katika mkutano wa klabu. Nenda mbele nafasi 2.

Ni wakati wa kupanda upya na huna mbolea yoyote ya asili tayari kwa kutumia. Rudi nyuma nafasi 4.

Mimea yako ya kabichi inashambuliwa na wadudu kwa sababu umeshindwa kupanda aina mbalimbali za mboga katika eneo moja. Anza upya shuleni.

Umesaidia kila mmoja kwenye shughuli zao za bustani ili muweze kurudi nyumbani pamoja. Nenda mbele nafasi 3.

Umeanza kucheza mpira wa miguu kabla ya shughuli za bustani kuisha. Rudi nyuma nafasi 3.



Nyumbani

MALIZA



Umeonesha namna ya kutunza kumbukumbu katika mkutano wa klabu. Nenda mbele nafasi 2.

Umegombea uongozi katika klabu yako ya 4-H. Nenda mbele nafasi 2.

Kabichi zako zina wadudu. Umenyunyizia dawa za kuulia wadudu za dukani kwenye bustani yako. Rudi nyuma nafasi 4.

Umeanza shughuli za 4-H nyumbani. Nenda mbele nafasi 3. Umeshindwa kuweka kumbukumbu. Rudi nyuma nafasi 2.

Baada ya kuvuna karoti, haraka umeongeza mbolea ya asili na kupanda pilipili hoho. Nenda mbele nafasi 2.

Unasumbua wakati wa mkutano wa klabu za 4-H. Rudi nyuma nafasi 1.

Umetengeneza ratiba ya kutunza bustani ya shule wakati wa likizo. Nenda mbele nafasi 4.

Umewanyang'anya wasichana vifaa vya bustani na kuvitumia wewe mwenyewe. Hii inapelekea wasichana kuchelewa kumaliza kupalilia. Rudi nyuma nafasi 2.

